# MACHAME HEALTH TRAINING INSTITUTE

**P.O. Box 3044, MOSHI** **Telephone: 2756873**
***E-mail: info@mhti.ac.tz*** ***MOSHI– TANZANIA***

**Our Ref. No: MHTI/COTC/01/VOL.IV/51** **Date: 15/09/2017**

Kwa Mzazi/Mlezi/Mfadhili ..... .....

**YAH: MAFUNZO KATIKA KOZI YA UUGUZI NGAZI YA STASHAHADA (DIPLOMA) 2017/2018**

Napenda kukuarifu ya kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Uuguzi katika Chuo cha Uuguzi Machame na mafunzo haya ni ya miaka mitatu. Hongera sana!

***Chuo kitafunguliwa tarehe 25/09/2017 na mwisho wa mwanafunzi kuripoti chuoni ni tarehe 12/10/2017 saa tisa na nusu mchana, mwisho wa kazi. Baada ya hapo nafasi yako itahesabiwa imepotea na kujazwa na mwombaji mwingine.***

Utaratibu wa malipo ni kama inavyojieleza hapo chini:-

| **DESCRIPTION** | **1ST YEAR** | **DESCRIPTION** | **2ND YEAR** | **DESCRIPTION** | **3RD YEAR** |
|---|---|---|---|---|---|
| TUTION FEE | 1,540,000 | TUTION FEE | 1,740,000 | TUTION FEE | 1,740,000 |
| REGISTRATION FEE | 70,000 | BORDING & LODGING | 1,425,000 | BORDING & LODGING | 1,425,000 |
| BORDING & LODGING | 1,425,000 | HEALTH INSURANCE | 50,400 | HEALTH INSURANCE | 50,400 |
| HEALTH INSURANCE | 50,400 | NACTE FEE | 15,000 | NACTE FEE | 15,000 |
| IDENTITY CARD | 20,000 | STUD. ASSOCIATIONS | 15,000 | STUD. ASSOCIATIONS | 15,000 |
| NACTE FEE | 15,000 | SPORTS | 15,000 | SPORTS | 15,000 |
| STUD. ASSOCIATIONS | 15,000 | **TOTAL** | **3,260,400** | GRADUATION | 110,000 |
| SPORTS | 15,000 | | | EXAMINATION FEE | - |
| **SUB TOTAL** | **3,150,400** | | | EXAM /LICENCING TNMC | 8 0,000 |
| UNIFORM | 75,000 | | | **TOTAL** | **3,450,400** |
| **TOTAL** | | | | | |
| | **3,225,400** | | | | |

Ada ya chuo kwa mwaka huu wa masomo 2017/2018 ni sh. 3,150,500/= (million tatu laki moja elfu hamsini na mia nne tu). Ambayo mchanganuo wake ni kama unavyoonekana kwenye jedwali. Ili kuthibitisha ukubali wako utatakiwa kulipa sh. 500,000 (laki tano tu) ambayo itakuwa ni sehemu ya malipo yako ya ada.

Ada hiyo ya Chuo inaweza kulipwa yote wakati mmoja, au nusu yake tunapofungua chuo, na nusu iliyobaki ilipwe tukifungua chuo muhula wa pili.

Ada ya chuo iingizwe kwenye akaunti ya chuo na mwanafunzi aje na Pay In Slip ya benki.

**Uchumi Benki**
**Jina la akaunti – Machame Health Training Institute**
**Akaunti namba – 001020000000555 - kwa wanaotoka Moshi**

**CRBD Benki**
**Jina la akaunti – Machame Health Training Institute**
**Akaunti namba – 0150206907200**

Ni lazima ada ya chuo ilipwe kikamilifu kama inavyotakiwa kila mwaka au muhula wa masomo, ambaye hakufanikiwa kumaliza ada husika hataruhusiwa kuendelea na masomo katika mwaka mpya wa masomo mpaka atakapomaliza ada husika.

Hautaandikishwa hapa chuoni kama ada ya chuo haikulipwa kwa utaratibu uliotajwa hapo juu. Kama mwanafunzi atafukuzwa katika chuo hiki kwa kosa lolote lile kulingana na sheria za chuo, ada haitarudishwa kabisa.

**MALIPO YANAYOTAKIWA KULIPWA WIZARANI MOJA KWA MOJA**

- Malipo ya Fedha kiasi cha 150,000/= kwa ajili ya Ada ya mitihani ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kila mwaka wa masomo utakayokuwa chuoni kwa account no**: "Application and Examination fee"Account N0. 20110007946. National Micro Finance Bank (NMB), iliyopo NMB Bank House** na pay-slip zitakusanywa chuoni baada ya malipo na kupelekwa wizarani kwa pamoja.
  Mwisho wa kulipa fedha hii ni tarehe 15/01/2018.
- 80,000 kwa ajili ya ada ya usajili katika baraza la wauguzi na ukunga Tanzania (The Nurses and Midwives Council)
- Kila somo la marudio (supplementary) litalipiwa 70,000/= (elfu sabini) katika akaunti ya chuo kabla ya kufanya mtihani husika.

## MAHITAJI YA CHUO

### A: SARE ZA WASICHANA:

- Magauni mawili ya rangi ya pinki (mikono mifupi) yatashonwa chuoni
1. Viatu vyeupe vyenye visigino Vifupi na visisababishe sauti/ usumbufu unapotembea.
- Soksi nyeupe

### SARE YA WAVULANA

- Suruali mbili rangi nyeupe - zitashonwa chuoni
- Mashati mawili meupe (mikono mifupi) yatashonwa chuoni

2. Viatu vyeupe vyenye visigino vifupi na visisababishe sauti/ usumbufu unapotembea.
- Soksi nyeupe

**C: MAHITAJI MENGINE:**

1. Godoro la futi sita kwa tatu
2. Blanketi, mto foronya na shuka za pink wasichana na light blue wavulana
3. Vifaa vya michezo
- Bukta
    - Fulana
    - Viatu vya michezo
4. Taulo
5. Ndoo moja ya plastic
6. Mwamvuli na sweta ya rangi ya pink kwa wasichana na nyeupe kwa wavulana.
7. Picha mbili za passport size (stamp size)
8. Tochi
9. Saa ya mshale yenye mshale wa sekunde
10. Futi kamba au tape measure
11. Utapimwa afya yako (medical examination) katika hospitali ya machame baada ya kufika chuoni
12. Utatakiwa uje na vyeti halisi **(ORIGINAL CERTIFICATES)** vya kidato cha nne na (siyo vivuli)
13. Kila mwanafunzi ni lazima ajiunge na Bima ya Afya ya Taifa.
14. Pia mwanafunzi atatakiwa kuja na **Ream 1 A4** kwa kila muhula ya karatasi za mitihani ya ndani.
15. LAPTOP kwa ajili ya masomo

**NB**:- Simu ya mkono hairuhusiwi darasani wala wodini wakati wa mazoezi

**UFUATAO NI UTARATIBU WA MAVAZI KWA MWANAFUNZI AWAPO CHUONI**

**<u>WANAFUNZI WA KIKE</u>**

1. Wavae sketi au gauni isiyo ya kubana na iwe ndefu ya kuvuka magoti akiwa amekaa.
3. Ni marufuku kuvaa <u>suruali</u> au <u>kaptula</u> wakati wowote uwapo chuoni.
4. Nywele bandia au zilizopakwa rangi haziruhusiwi kabisa
5. Hereni , Bangili, Mikufu, Pete ambazo si za ndoa pamoja na manukato yenye harufu kali haviruhusiwi.
6. Wavae uniform (sare) pamoja na vitambulisho wakati wote wa madarasa, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo.
7. Kucha ndefu na rangi haziruhusiwi kabisa
8. Meno ya dhahabu hayaruhusiwi

**WANAFUNZI WA KIUME**

1. Ni marufuku kufuga nywele ndefu, rasta, ndevu na usinyoe zungu la unga (kipara)
2. Kucha/ukucha haviruhusiwi kwa wote
3. Mikufu ,Pete, zisizo za ndoa haziruhusiwi kabisa
4. Meno ya dhahabu hayaruhusiwi
5. Wote wavae uniform (sare) pamoja na vitambulisho wakati wote wa madarasa, mawodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo.

**KIELELEZO CHA JINSI YA KUFIKA CHUO CHA AFYA MACHAME**




NAKUTAKIA KILA LA KHERI KATIKA MASOMO WAKATI WA MAFUNZO HAYO

# KARIBU CHUO CHA AFYA MACHAME

……

**AQWILINER KWAY**
**MATRON**
**SIMU: 0784 695521**

……

**MWELINDE JASSON**
**MLEZI WA WANAFUNZI**
**SIMU: 0769 141427**